Toleo 44

# Ukweli wa Injili

Mafundisho ya Biblia na Himizo kwa Kazi ya Kimisheni Ulimwenguni Kote

## VAENI SILAHA ZOTE ZA MUNGU

*Vaeni silaha zote za Mungu, mpate kuweza kuzipinga hila za Shetani.* — Waefeso 6:11

Mungu ametupatia uwezo kwa njia ya Mwanaye Yesu Kristo na kwa nguvu za Roho Mtakatifu, ili sisi kama watoto wake tuweze kuishi maisha ya ushindi na ya kiungu. Kuna vita vya kiroho ambavyo vinaendelea, na watu wanahadaliwa na kushindwa na nguvu za Ibilisi. Watu wengi wanaojiita Wakristo wanaishi maisha ya dhambi na katika hali ya kushindwa. Lakini habari njema za injili ni kwamba, Mungu ametupatia uwezo kwenye kizazi hiki chetu wa kuweza kushinda dhambi, na unaotuwezesha kuishi maisha ya kila siku kw a ushindi na furaha.

Lakini ili mwanajeshi wa msalaba aweze kuishi katika hali ya ushindi, anahitaji kuvaa silaha zote za Mungu, ndiposa aweze kukataa na kushinda hadaa zote na nguvu za yule Mwovu. Kwa kweli Mungu hajatuacha bila silaha, bali Yeye ametupatia vifaa vya kivita vya kutuwezesha kusonga mbele, na kupata ushindi dhidi ya nguvu ZOTE za adui.

Lakini ikiwa askari atasahau kuchukua moja ya silaha zake, au pengine asahau kuchukua baadhi ya vifaa vyake vya kujikinga, na kukosa kwenda navyo vitani, inakuwa kwamba yeye amejiweka wazi kwa uvamizi wa adui, na hana silaha tosha za kupigana. Ni vivyo hivyo kwa Mkristo. Ni lazima tutafute na tupate kila uwezo ambao Mungu ametupatia; na kwa njia hiyo tutaweza KUSIMAMA wima kwa uaminifu, kwa njia ya kufuata ukweli, na kwa ushindi. Waefeso 6:14-17 imetoa maelezo ya silaha zote za Mungu.

**Mkanda wa Ukweli:** Mkanda (au mshipi) wa askari wa Kirumi ndio ulidumisha silaha zake mahali panapofaa. Ukweli wa Neno la Mungu, ambao ni wa kudumu, unamfunga kila mtu, na hauna mwisho, na ndio utatuongoza hadi Mbinguni. Shetani ni mwongo, na anafanya kazi yake duniani, na hata ndani ya kanisa na manyumbani. Lakini ukweli mtakatifu wa Neno lake Mungu ndio ambao unaweka wazi hadaa za adui, na kutupatia mwangaza wakati tunapokuwa gizani. Ukweli ulioingizwa uongo ndani yake ndio ambao unazaa Wakristo dhaifu, na kuleta hali ya kushindwa. Lakini ukweli safi unaleta uwezo na nguvu kwa mtu wa Mungu, na kumpatia silaha za kuweza kupigana na uongo wa ulimwengu ambao ni mharibifu, na hata wa dini za uongo.

**Utakatifu Kama Vazi la Kujikinga Kifuani:** Silaha hii ya kujikinga ndio ambayo ilimlinda askari kifuani na moyoni. Utakatifu wa Kristo ukiwa ndani yetu ndio unatoa usalama na kudumisha maisha yetu ya kiroho. Tukipata tulizo katika haki yake Mungu, badala ya kujaribu kuipata kutokana na nguvu zetu wenyewe, ndiko kunakotuwezesha kuishi maisha matakatifu katika ulimwengu huu mwovu. Ndani yake Kristo mtoto wa Mungu ataweza kufanya maamuzi ambayo yatakuza usalama wa kiroho, na ambao pia utamkinga dhidi ya uchafu wa ulimwengu ili usiingizwe ndani yake. Askari wa Kristo hawezi kudumu nje ya haki, kwa sababu akifanya hivyo atazidiwa na dhambi.Wakati Wakristo wamelinda mioyo na mawazo yao na kumpenda Mungu na njia zake za utakatifu (zaidi ya kitu kingine chote) ndipo wataweza kushinda tamaa za ulimwengu.

**Viatu vya Injili ya Amani:** Viatu ndivyo ambavyo vilipatia miguu usalama wakati askari walipofanya safari ndefu. Mahali pote ambapo Wakristo wanatemba wanastahili kwenda na habari njema za

*(Endelea katika Ukurasa 2)*



"Mungu ametupatia uwezo kwenye kizazi hiki chetu wa kuweza kushinda dhambi, na unaotuwezesha kuishi maisha ya kila siku kw a ushindi na furaha."


| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| Taharir | Mafundisho ya Biblia: Kutubu | Toba Ambayo Inafundishwa Katika Biblia | Maswali na Majibu | Je, Wajua? Neno Linalofaa kwa Msimu Huu |
| 3 | 4 | 5-6 | 7 | 8 |

# MAMBO AMBAYO BIBLIA INAFUNDISHA KUHUSU...

**Neno la Mungu**
2 Tim. 3:6, 2 Pet. 1:20-21, Mt. 24:35

**Uhusiano wa Upendo**
Mt. 22:37-40, Yn. 14:21-23, 1 Yoh. 4:7-21

**Toba**
Mdo. 3:19, 17:30, 2 Kor. 7:10

**Uzao Mpya**
Yn. 3:3-7, 2 Kor. 5:17, Rum. 6:1-4, Efe. 2:1, 5-6

**Uhuru Kutokana na Dhambi**
1 Yoh. 5:18, Mt. 1:21, Yn. 8:11

**Ujazo wa Roho Mtakatifu**
Mdo. 19:2, 15:8-9, 1:8

**Utakatifu**
Lk. 1:73-75, Ebr. 12:14, 1 Pet. 1:15-16, Tit. 2:11-12, Rum. 6:22

**Ufalme wa Mungu**
Lk. 17:20-21, Rum. 14:17, Yn. 18:36

**Kanisa**
Mdo. 2:47, Efe. 4:4-6, 1 Kor. 12:12-13, Kol. 1:18

**Umoja**
Yn. 17:20-23, Gal. 3:28, Ufu. 18:2-4

**Kanuni za Kanisa**
Mt. 28:19-20, 26:26-30, I Kor. 11:23-27, Yn. 13:14-17

**Uponyaji wa Kiungu**
Lk. 4:18, Isa. 53:4-5, Yak. 5:13-16

**Utakatifu wa Ndoa**
Mt. 19:5-6, Lk. 16:18, Rum. 7:2-3, I Kor. 7:10-11

**Urembo wa Nje**
I Tim. 2:9-10, I Kor. 11:14-15, Kum. 22:5

**Mwisho wa Nyakati**
2 Pet. 3:7-12, Yn 5:28-29, 2 Kor. 5:10, Mt. 25:31-46

**Kupenda Amani**
Lk. 6:27-29, 18:20

**Ibada**
Yn. 4:23-24, Efe. 5:19, 2 Kor. 3:17

**Wajibu Mkuu**
Mk. 16:15

*(Inaendelea kutoka Ukurasa 1)*

injili. Yesu ndiye chanzo cha amani, na amani hiyo inahitaji kuzingira na kujaza mioyo yetu. Zaidi ya hayo, watoto wa Mungu wanahitaji kutafuta amani katika mahusiano yote na wanadamu wenzao. Hii ni kwa sababu mahusiano yasiyofaa yamewafanya Wakristo wengi kuanguka. Basi hebu vaa katika miguu yako injili ya amani, na utafute masikizano (badala ya ugomvi na migogoro) kati yako na familia yako, na hata na majirani zako.

**Ngao ya Amani:** Ngao ya askari wa Kirumi ilikuwa na urefu wa futi nne. Na ngao hiyo ndiyo ilimlinda askari kutokana na mishale na mikuki ya adui. Imani kwa Mungu huwa ni ngao inayotupatia usalama kutokana na mavamizi yake Ibilisi. Wakati tumekumbana na majaribu, masumbufu, na ugumu wa aina zote, hebu tuinue ngao ya amani na tudumishe tumaini na ujasiri wetu kwa Mungu, kwa upendo wake, na kwa ukweli kwamba Yeye ndiye anayekutana na mahitaji yetu.

**Kofia ya Wokovu (iliyoundwa kwa chuma):** Kofia hii ambayo ilikuwa muhimu kabisa vitani ilimkinga askari kichwani na usoni. Wokovu ni kipawa kutoka kwa Mungu, na ni kwa neema na nguvu zake tu ndipo tunaweza kuishi kwa ushindi. Wakati tumeokoka tunaweza kuishi kwa ujasiri tukiwa na hakikisho kwamba tumepewa usalama na nguvu kutoka kwa Mungu wetu. Kamwe sasa hatuongozwi na dhambi, mwili, au na watu wanaotuzunguka. Tumelindwa na tuko na usalama kwa jinsi tutaendelea kutumaini kazi zake Mungu, ambayo ni za kiungu.




**Upanga wa Roho:** Upanga ulikuwa ni silaha ya kumshambulia adui wakati wa vita. Askari hastahili tu kuishi maisha ya kujilinda, badala yake anahitaji kusonga mbele na kumsukuma adui ili adui huyo amwondokee. Mungu alitupatia Roho Mtakatifu ili kumwezesha mtoto wa Mungu kumshinda adui, na ndiposa aweze kusonga mbele. Upanga wa Roho ni "Neno la Mungu"; maanake Biblia pamoja na neno linalotamkwa kwa uwezo wake Roho Mtakatifu. Hiki ndicho kitu ambacho kinatupatia nguvu kumshinda adui, kama vile ambavyo Yesu Mwenyewe alitumia Maandiko kumshinda Ibilisi wakati alijaribiwa huko jangwani.

Mungu hakutupatia jukumu la kuishi maisha matakatifu yanayolingana na ya Kristo bila ya Yeye kutupatia kila chote tulichohitaji cha kutuwezesha kushinda nguvu za adui. Basi hebu wewe Mkristo usitekwe na mawazo na falsafa za ulimwengu, na pia usiamini itikadi za vikundi vya kidini, badala yake chukua silaha zake Mungu. Wale walioshindwa, waliorudi nyuma, na hata wale ambao tayari wamepata majeraha ya dhambi na nguvu za kimwili wanaweza kuinuka tena na kuishi maisha ya ushindi kwa nguvu zake Mungu. Kusema kweli sisi tuna tumaini na ushindi wa ajabu! ■

Gazeti la *Ukweli wa Injili* ni jalida ambalo linatolewa kila robo ya mwaka kwa manufaa ya Kanisa la Mungu kwa ajili ya mafundisho na kwa ajili ya kuwahimiza Wakristo ili washike kweli za Biblia. Tutembelee katika tovuti yetu ya *www.thegospeltruth.org* na ujiandikishe ili uwe ukitumiwa notisi kwa njia ya barua pepe kila wakati jalida hili likiwa tayari ili uweze kupata toleo la kila kipindi. Gazeti hili la *Ukweli wa Injili* linachapishwa katika nchi nyingi ili lisambazwe katika nchi hizo. Kazi hii inawezekana kupitia kwa matoleo yanayotolewa kwa hiari. Pia wewe ukitaka unaweza kutumiwa risiti ya vile tumelipa ushuru kutokana na zawadi yako.

—Mhariri, Michael Smith

Gospel Truth, P.O. Box 2042, Nixa, MO 65714 USA
editor@the gospeltruth.org

# Tahariri



*Uwafumbue macho yao, na kuwageuza waiache giza na kuielekea nuru, waziache na nguvu za Shetani na kumwelekea Mungu; kisha wapate msamaha wa dhambi zao, na urithi miongoni mwao waliotakaswa kwa imani iliyo kwangu mimi.* —Matendo 26:18

Yesu alikutana na Sauli wakati Sauli akiwa njiani kuelekea Dameski. Ndipo Sauli akamuuliza, "Wewe u nani, Bwana?" Naye Yesu akamjibu, "Mimi ni Yesu (Matendo 26:15). Hapo Yesu akaanza kumweleza Sauli kile ambacho alikuwa amemwitia, na mpango wake wa kiungu juu ya maisha yake. Yeye alipewa jukumu la kuhubiri Injili ili macho ya watu yaweze kufunguliwa, na ili kwamba wabadilike "waziache nguvu za Shetani na kumwelekea Mungu." Ndiposa sisi tunasema haleluya! Huu ungali ndio ujumbe wa Injili hata katika siku hizi zetu. Nguvu za Shetani zimevunjwa; na kuna ukombozi na ushindi ambao mwenye dhambi na mwenye kurudi nyuma anaweza pata.

Mimi naandika toleo hili la Ukweli wa Injili ambalo linahusu somo la Mkristo kuishi maisha ya ushindi huku nikiwa na furaha na machozi mengi. Hii ni kwa sababu idadi kubwa mno ya watu inaendelea kuishi dhambini na katika hali ya kufa moyo huku wakijaribu kuachana na dhambi. Wao wanajaribu na kushindwa na pia kulemazwa na uraibu wa aina tofauti tofauti, na pia umwili wao, nayo imani yao inazidi kudidimia. Katika siku hizi zetu watu wengi hawaamini kwamba kuna ujuzi wa wokovu ambao mtu anaweza kuupata katika maisha yake kibinafsi. Lakini hebu wewe ufurahi pamoja nami unapolisoma gazeti hili. Hii ni kwa sababu kungali kuna ukombozi wa kumwezesha mtu kutoka dhambini, na pia kungali kunapatikana nguvu za kushinda majaribu. Mungu angali ana uwezo, na pia angali anafanya kazi yake ya kubadilisha maisha ya watu.

*Tutembelee www.thegospeltruth.org ili kujiandikisha na kupata jarida za mbele.*

Hebu tafakari kuhusu maneno ya ajabu ambayo yanapatikana katika wimbo wa Lewis E. Jones unaojulikana kama *Kuna Uwezo wa Ajabu Damuni.*

Uwe huru kutoka dhambini,
Uko uwezo, wa ajabu;
Juu ya uovu uwe mshindi,
Damuni mwa Mwana-Kondoo

Kukariri/Pambio:
Uwezo, wa, ajabu ndimo
Damuni, mwa Yesu,
Uwezo, wa, ajabu ndimo
Damuni mwa Mwana-Kondoo.


Hakuna haja ya sisi kuendelea kuzama katika utumwa wa dhambi. Badala yake tunahitaji kuishi kwa uhuru kupitia kwa nguvu za damu. Mimi ninamshukuru Mungu kwa ukweli huo. Mwandishi mmoja stadi wa nyimbo aliandika na kusema, "Mimi ni mwenye dhambi tu, ambaye ameokolewa kwa neema." Lakini mimi mwenyewe ninamshukuru Mungu kwa ukweli kwamba wokovu wangu haulingani na maneno hayo. Mimi NILIKUWA mwenye dhambi, lakini sasa mimi sio mwenye dhambi tena, kwa sababu Yesu aliniinua na kunitoa dhambini.

Mpango wa Mungu ni mzuri na unatosha. Kama mtu anaishi maisha ambayo hayana ushindi hii haitokani na ukosefu wa nguvu zake Mungu. Watu wengi huanguka dhambini kwa sababu ya kukosa kumtafuta Mungu ili wapate ujazo wa Roho Mtakatifu. Mimi nina hakika kwamba hii ni moja ya haja kubwa sana kati ya Wakristo wa siku zetu. Wakristo wanahitaji kujitoa mhanga katika madhabahu ya kujitolea kwa Mungu ili waweze kujazwa moto na nguvu za Roho Mtakatifu. Nguvu za Roho Mtakatifu ndizo zinamwezesha mtu kusimama wima, na pia kumsaidia Mkristo kuishi maisha yake ya kila siku yanayompendeza Bwana. Hili ndilo suluhisho la aina ya maisha ambayo Wakristo wengi wanaishi leo, maisha ya kusimama, tena kuanguka, kusonga mbele kidogo, tena kurudi nyuma.

Basi tunaomba kwamba Bwana atakubariki wewe unapojifunza kuhusu thiolojia hii ya mafundisho haya. Lakini zaidi ya yote, hebu wewe upate himizo na changamoto la kufungua moyo wako ili uweze kuishi maisha haya ya ushindi.

Michael W. Smith

Aprili 2023





# Mwongozo wa Kujifunza Biblia

## Somo: Kuishi Maisha ya Ushindi Kama Mkristo

**Somo la Maandiko:** *Lakini Mungu na ashukuriwe atupaye kushinda kwa Bwana wetu Yesu Kristo.* —1 Wakorintho 15:57

**Muhstasari:** Kuna ujuzi wa maisha ambao unaweza patikana kupitia kwa mpango wa wokovu wa Mungu ambao unamwezesha Mkristo kudumisha maisha ya ushindi; na pia kumwezesha kudumisha maisha yake yasiingie dhambini, au yeye kujihusisha na mambo ya kidunia.

### I. Uhuru kutokana na Dhambi

A. Warumi 6:1-2 Tudumu katika dhambi?
B. Warumi 8:3 Yale yasiyowezekana kwa sheria.
C. Mathayo 1:21 Yesu aokoa kutoka dhambini.
D. 2 Wakorintho 5:17 Ya kale yamepita.
E. Warumi 6:6-7 Mwili wa dhambi umebatilika.

### II. Nguvu za Kuishi Bila Kutenda Dhambi

A. 1 Yohana 1:7 Tumesafishwa dhambi yote.
B. 1 Yohana 3:6-8 Ibilisi hutenda dhambi.
C. 1 Yohana 5:18 Aliyezaliwa na Mungu.
D. Warumi 6:12-14 Dhambi isitawale ndani ya miili yenu.
E. 1 Wakorintho 6:9-11Sasa nyinyi sio watu wasiokuwa wa haki.

### III. Maagizo Kwamba Tusitende Dhambi

A. Yohana 8:11 Enenda zako; wala usitende dhambi tena.
B. 1 Wakorintho 15:34 Msitende dhambi. (1 Yohana 2:1).
C. Tito 2:11-12 Tukatae ubaya / tupate kuishi kwa utauwa.
D. 1 Petero 2:21-22 Tufuate mfano wa Kristo: kwa kutotenda dhambi.

### IV. Nguvu za Roho

A. Luka 24:49 Mvikwe uwezo.
B. Matendo 1:8 Roho Mtakatifu hupeana nguvu.
C. Yohana 14:26 Roho Mtakatifu hufariji na kufundisha.
D. Zekaria 4:6 Ushindi kwa Roho wake Mungu

### V. Ahadi za Mungu


A. Yohana 8:36 Mtakuwa huru kweli kweli.
B. 1 Yohana 5:4-5 Kushinda kuushindako ulimwengu.
C. Luka 10:17 Hata pepo wanatutii.
D. 1 Wakorintho 10:13 Mweze kuepuka majaribu.
E. Zaburi 44:3 Ushindi kwa mkono wa Mungu.
F. Wafilipi 4:13 Mambo yote katika Kristo.
G. Kumbukumbu 20:4 Mungu atawapigania.
H. 1 Yohana 4:4 Ni mkuu kuliko.
I. Yohana 16:33 Kristo ameushinda ulimwengu.

Tamati

*Lakini katika mambo hayo yote tunashinda, na zaidi ya kushinda, kwa yeye aliyetupenda.*
—Warumi 8:37

## Ni kwa nini Yesu aliwaambia watu “WAENDE NA WASITENDE DHAMBI TENA” kama haingewezekana wao kuishi maisha yasiyo na dhambi?

# KUISHI MAISHA YA UKRISTO YENYE USHINDI



Je, tuendelee kutenda dhambi? Je, inabidi sisi kuendelea kujisalimisha kwa majaribu ya Ibilisi? Je, ni lazima kila wakati tuendelee kudumu katika hali ya kuanguka na kushindwa maishani mwetu kama Wakristo? LA hasha! Hebu tumshukuru Mungu kwa sababu tunaweza kupata ujuzi huo wa kuwa washindi, na tunaweza pia kupata nguvu za kushinda kwa njia ya Bwana wetu Yesu Kristo.

"Neno la Mungu linasema hayo kwa njia ya wazi kabisa: 'Damu yake Yesu, Mwana wake, yatusafisha dhambi yote.' "

## Wokovu wa Kutoka Dhambini

Mtume Paulo aliuliza swali hilo katika Warumi 6:1-2, "Tudumu katika dhambi ili neema izidi kuwa nyingi? Hasha!" Lakini asilimia kubwa sana ya Wakristo katika ulimwengu wa sasa wa Kikriso wanasema kwamba INATUBIDI tuendelee kutenda dhambi kila siku, aidha ziwe nyingi au chache. Wao wanadunisha dhabihu ya Kristo, na kudai kwamba ilikuwa ni ya kuleta msamaha wa dhambi peke yake, na wanakosa kutambua na kukubali neema ya ukombozi ambayo humwinua mwanadamu kutoka katika hali yake ya dhambi, na kumleta katika hali ya ushindi kupitia kwa nguvu za damu ya Yesu. Warumi 8:3 insema, "Maana yale yasiyowezekana kwa sheria, kwa vile ilivyokuwa dhaifu kwa sababu ya mwili, Mungu, kwa kumtuma Mwanawe mwenyewe katika mfano wa mwili ulio wa dhambi, na kwa sababu ya dhambi, aliihukumu dhambi katika mwili." Wakati wa kipindi cha Sheria ya Musa haingwezekana wanadamu kuishi bila kutenda dhambi—maanake kutokwenda kinyume na maadili, jambo ambalo ndilo humtenga mwanadamu na Mungu. Lakini Yesu alikuja ili kufanya kile ambacho sheria haingefaulu kufanya. Hata jina halisi la Yesu linasema kuhusu mpango wa kweli wa wokovu, "Maana, yeye ndiye atakayewaokoa watu wake na dhambi zao" (Mathayo 1:21).

## Kuna Ukombozi

Walimu na vikundi vya kidini (vya uongo) hupungunza mpango huo mkuu wa wokovu na kuufanya uwe tu ni kwamba Kristo aliwaokoa watu wake huku wakiwa wangali NDANI ya dhambi zao. Naye Ibilisi na wajumbe wake wanaendeleza mafundisho haya ya uongo ili kwamba watuibie tumaini la kweli na furaha ya wokovu wa kweli. Lakini hebu tumshukuru Mungu kwa sababu tunaweza okolewa kutokana na nguvu za dhambi na kuweza kuishi katika haki na utakatifu. Kwa njia ya wazi kabisa maandiko yanafundisha kuhusu maisha ya ushindi na ukombozi kutoka utumwani. "Hata imekuwa, mtu akiwa ndani ya Kristo amekuwa kiumbe kipya; ya kale yamepita tazama! Yamekuwa mapya" (2 Wakorintho 5:17). Tabia za kale, uraibu na kushiriki mambo tofauti tofauti ambayo hayafai, tamaa za mwili, machungu, mambo yote ambayo yanawateka watu nyara na kuwadumisha ndani ya dhambi huweza kuvunjwa kwa nguvu zake Mungu. Dhambi huangamizwa na kushindwa na kufanya "Tusitumikie dhambi tena" (Warumi 6:6). Mkristo anaweza na hana budi kuishi maisha ya ushindi juu ya dhambi na utumwa. Haijalishi nguvu za dhambi zina uwezo mkubwa kiasi gani, kuna ukombozi unaopatikana katika wokovu huu wetu.

## Maisha Yaliyobadilishwa

Mtume Paulo alitambua dhambi za kale za wale walio-okoka katika 1 Wakorintho 6:9-11. Wengi wao walikuwa waasherati, waabudu sanamu, wazinzi, mashoga, wezi, walevi, n.k. "Na baadhi yenu mlikuwa watu wa namna hii; lakini mlioshwa, lakini mlitakaswa, lakini mlihesabiwa haki katika jina la Bwana Yesu Kristo, na katika Roho wa Mungu wetu." Hakuna mwenye dhambi atakayerithi ufalme wake Mungu. Wote wametenda dhambi, lakini maisha ya wanadamu hubadilishwa kwa nguvu zinazotoka kwa Mungu. Damu yake Yesu ina nguvu za kushinda nguvu za dhambi. Ni jambo la huzuni kwamba wengi wanaojiita Wakristo hawajapata ujuzi wa kweli wa wokovu. Ukweli ndio unabadilisha maisha ya wanadamu kabisa kabisa, na humwezesha mtu kushinda dhambi zote kwa neema yake Mungu! Neno la Mungu linasema hayo kwa njia ya wazi kabisa: "Damu yake Yesu, Mwana wake, yatusafisha dhambi yote" (1 Yohana 1:7).

*(Endelea katika Ukurasa 6)*

(Inaendelea kutoka Ukurasa 5)

## Usitende Dhambi

Dhambi huwa zinatokana na athari na nguvu za Shetani. Lakini Yesu alikuja dunia na akafa "ili azivunje kazi za Ibilisi" (1 Yohana 3:8). Mstari wa 6 unasema, "Kila akaaye ndani yake hatendi dhambi; kila . . . atendaye dhambi ni wa Ibilisi." Katika 1 Yohana 5:18 mtume huyu anatangaza kwamba "Twajua ya kuwa kila mtu aliyezaliwa na Mungu hatendi dhambi; . . . wala yule mwovu hamgusi." Hebu ulimwengu wote ujue kwamba katika kizazi hiki kungali kunapatikana maisha ya uhuru kutoka kwa dhambi, na kwamba nguvu za Shetani zimevunjwa kupitia kwa Kristo. "Kwa maana dhambi haitawatawala ninyi, kwa sababu hamwi chini ya sheria, bali chini ya neema" (Warumi 6:14). Kile ambacho kiliongoza na kutawala tabia za watu huku wakiwa wangali dhambini katika himaya ya sheria kimevunjwa nguvu zake kupitia kwa nguvu za ukombozi wa neema.



## Neema ya Mungu Ndiyo Inamwezesha Mwanadamu Kuishi Bila Kutenda Dhambi

Hata ingawa wanathiolojia wanaweza kugeuza na kufanya juhudi zote ili kutoa visingizio vya kutenda dhambi, Neno la Mungu linafundisha kuhusu maisha ya kila siku ya ushindi juu ya dhambi. Yesu mwenyewe alimwambia mwanamke aliyepatikana katika uzinzi, "Enenda zako; wala usitende dhambi tena" (Yohana 8:11). Yeye hakuwa akimwagiza kufanya kitu ambacho hangeweza kufanya, bali alikuwa akimpa tumaini na nguvu za kwenda zake na kuishi bila kuwa mfungwa tena wa matendo ya uzinzi ambayo alikuwa akifanya hapo mbeleni. Mtume Paulo naye anatoa mwongozo kama huo katika 1 Wakorintho 15:34, "Tumieni akili kama ipasavyo, wala msitende dhambi." Naye Petro anatuhimiza katika 1 Petro 2:21-22 kwamba tufuate nyayo za Kristo ambaye "hakutenda dhambi." Kwa kweli neema ya Mungu ambayo ilileta wokovu inatufundisha, "Kukataa ubaya na tamaa za kidunia; tupate kuishi kwa kiasi, na haki, na utauwa, katika ulimwengu huu wa sasa" (Tito 2:11-12). Haya ndio maisha ya ushindi.

> "Roho Mtakatifu ndiye humpatia Mkristo nguvu za kuweza kuwambia Ibilisi, mwili, na ulimwengu 'LA,' na pia kumwezesha mtu kupata nguvu za kumwambia Bwana 'NDIO.' "

## Wokovu Kamili

Wokovu ni ujuzi wa ajabu unaopatikana wakati mwenye dhambi amemwamini Kristo na kutubu dhambi zake, na pia kusamehewa na kutakaswa kwa damu yake Yesu. Sasa chombo hicho kinakuwa safi. Lakini Mungu anataka kujaza chombo hicho Roho Mtakatifu. Yesu aliwaambia wanafunzi wake, "Kaeni humu mjini (Yerusalemu), hata mvikwe uwezo utokao juu" (Luka 24:49). Vivyo hivyo Matendo 1:8 inasema, "Lakini mtapokea nguvu, akiisha kuwajilia juu yenu Roho Mtakatifu." Hili ni jambo muhimu linaloleta uwezo wa kumwezesha mtu kuishi maisha ya ushindi. Kujazwa Roho Mtakatifu ni sehemu muhimu ya mpango kamili wa wokovu. Roho Mtakatifu ndiye humpatia Mkristo nguvu za kuweza kuwambia Ibilisi, mwili, na ulimwengu "LA," na pia kumwezesha mtu kupata nguvu za kumwambia Bwana "NDIO." Roho Mtakatifu anafariji, anafunza, anaongoza, na hata anawapatia Wakristo nguvu (Yohana 14:26). Roho Mtakatifu akiwa ndani yetu ndiye atatupatia nguvu katika nyakati zetu za udhaifu, na hata kuipatia miili yetu nguvu za kudumisha ushindi na utakatifu maishani mwetu.

## Ahadi Tulizopewa Kama Waumini

Neno la Mungu limejaa ahadi ambazo zinatoa himizo kwa watoto wa Mungu wakati wakipambana na ulimwengu huu wa giza. Uhuru dhidi ya dhambi haitakiwi kuwa ni jambo ambalo si la kudumu, kwa sababu tumepewa ahadi kwamba, "Mwana akiwaweka huru, mtakuwa huru kweli kweli" (Yohana 8:36).

Tunaweza kupata ujasiri kutokana na ukweli kwamba, "Kilichozaliwa na Mungu huushinda ulimwengu" (1 Yohana 5:4-5). Maisha ya Mkristo sio ya kushindwa, na pia sio ya kuanguka. Alama halisi za Mkristo ni ushindi, nguvu, na kuweza kukua. Hatuna haja ya kuogopa wakati Shetani anapiga makelele kutokana na makasiriko yake, kwa sababu hata ibilisi hao hawana budi kuwa watiifu kwetu katika jina lake Yesu (Luka 10:17). Wakati majaribu yametujia kwa nguvu, na hatuoni njia ya kuepuka, Mungu ameatuahidi kwamba "atafanya na mlango wa kutokea" (1 Wakorintho 10:13). Wakati mwingine miili yetu inakuwa na udhaifu, na nguvu za adui yetu zinaweza kutujia kwa nguvu. Lakini wakati tumevaa silaha zake Mungu tunaweza kutegemea nguvu zake, na kuweza kufanya kile ambacho sisi wenyewe hatuna nguvu kujifanyia.

Wana wa Israeli hawakushinda nchi ya Kanaani kwa upanga wao wenyewe, bali kwa mkono wa kuume wa nguvu zake Mungu (Zaburi 44:3). Mungu atawapigania watoto wake (Kumbukumbu 20:4) na kuwahifadhi hadi mwisho. Tunaweza kutwaa ahadi zake Mungu, na kusema pamoja na mtume Paulo kwamba: "Nayaweza mambo yote katika yeye anitiaye nguvu" (Wafilipi 4:13). Basi hebu wewe upate faraja na uyafuatilie maisha hayo ya ushindi, hata katika wakati wa hali na hisia tofauti tofauti maishani mwako, kwa sababu "Yeye aliye ndani yenu ni mkuu kuliko yeye aliye katika dunia" (1 Yohana 4:4).

Yesu alifahamu kwamba ulimwengu huu ni wa giza, na kwamba kutakuwa na mvutano wa kutoka ndani yetu, na hata wa kutoka nje. Lakini Yeye akiwa ndiye mwenye kutupatia amani na ushindi anatutolea himizo linalotufaa hata katika siku hizi zetu, kwamba: "Ulimwenguni mnayo dhiki; lakini jipeni moyo; mimi nimeushinda ulimwengu. (Yohana 16:33). Kuna amani, ushindi, na nguvu zinazopatikana juu ya dhambi za aina zote, na kila siku tunaweza kuishi maisha ya ushindi kwa sababu, "Tunashinda, na zaidi ya kushinda, kwa yeye aliyetupenda" (Warumi 8:37).

"Ee Bwana, twaomba kwamba tusiwahi tosheleka katika hali yetu ya kushindwa au katika kuanguka kwetu, bali kwamba tutainuliwa kwa nguvu zake Yesu, na kwa Roho Mtakatifu, ili tuweze kuombea na hata tupate hayo maisha ya ajabu ya ushindi, ambayo yanapatikana ndani yako pekee ee Yesu. Amina." ■

# Maswali na Majibu



## Ni nini maana kamili ya mtu kuishi akiwa huru kutokana na dhambi

Wakati mtu ameokoka, Maandiko yanasema kwa uwazi kwamba kuna nguvu za kumwezesha kuishi bila kutenda dhambi. “Kila mtu aliyezaliwa na Mungu hatendi dhambi” (1 Yohana 3:9). Wakati watu wanajadili kuhusu mambo ya dhambi ni muhimu wao kujua na kuelewa maana yake kamili.

Agano Jipya linatoa maana nne za kimsingi za dhambi—mambo ambayo yanamtenga mwanadamu kutoka kwa ushirika na Mungu. Mtoto wa kweli wa Mungu anaishi bila kwenda kinyume cha Maandiko yafuatayo.

“Kila lisilo la haki ni dhambi” (1 Yohana 5:17).

“Kila atendaye dhambi, afanya uasi” (1 Yohana 3:4).

“Basi yeye ajuaye kutenda mema, wala hayatendi, kwake huyo ni dhambi” (Yakobo 4:17).

“Na kila tendo lisilotoka katika imani ni dhambi” (Warumi 14:23).

Ili tuseme kwa uwazi zaidi kuhusu swala hili, hebu tuongee kuhusu Sheria ya Musa, kwamba, “Hivyo torati imekuwa kiongozi kutuleta kwa Kristo” (Wagalatia 3:24). Wakati mwanadamu alikuwa chini ya utawala wa sheria yeye hangeweza kudumisha maisha ya ushindi juu ya dhambi. Hebu tafakari kuhusu Daudi, ambaye alitenda uzinzi, na kuhusu Abrahamu, ambaye alisema uongo. Mioyo yao ilitaka kumtumikia Mungu, lakini hawakuwa na uwezo wa kuishi pasi kutenda dhambi, ndiposa wakategemea kafara za wanyama kulingana na sheria ya Mungu, ndiposa waweze kusamehewa. Lakini katika Agano Jipya, kuna nguvu ndani ya damu ya Yesu, sio tu kwa ajili ya mtu kupata msamaha, bali pia kwa ajili ya yeye kuweza “kwenenda bila kutenda dhambi.” Mungu alitoa Sheria ili kutujulisha dhambi ni nini, ili tuweze kuielewa, na kupata kujua kwamba hatuwezi kuishi bila kutenda dhambi kwa nguvu zetu za kibinafsi. Kwani “Kutambua dhambi huja kwa njia ya sheria” (Warumi 3:20).

Lakini katika Agano Jipya dhambi ni swala la moyo, na ni uasi dhidi ya Mungu na njia zake, kwa maana kupitia kwa Kristo TUNAWEZA kuishi bila kuivunja sheria. Hebu tuzingatie kwamba, Mitume Paulo na Yohana wanaposema kuhusu wale ambao hawatafika Mbinguni wanataja maovu kadhaa kwa njia ya wazi kabisa—ibada ya sanamu, uasherati, uzinzi, kusema uwongo, kuiba, ulevi n.k. Mambo haya ndio mtu akitenda huwa anaenda kinyume na MAADILI, na ndio yanatenganisha Mungu na mwanadamu. Hizi ndizo dhambi.

## Je, mtu kuishi maisha ya ushindi juu ya dhambi nikumaanisha kwamba yeye hatawahi kufanya makosa au kupungukiwa?

Hili ni swali muhimu kabisa kwa jambo hili tunalojadili. Mimi sijawahi kutana na Mkristo aliyeokoka na pia kujazwa Roho Mtakatifu, na ambaye hajawahi fanya makosa au kupungukiwa. Lakini kuna tofauti kati ya kutenda dhambi ikilinganishwa na swala la kufanya makosa au kupungukiwa. Wakristo hawana budi kumpenda Mungu kuliko mambo mengine yote; na lengo na shauku la maisha yao linahitaji kuwa ni wao kufanyika kuwa kama Kristo. Hii si kumaanisha kwamba sisi kama wanadamu tu wakamilifu. Kwa kweli sisi hatufanyi mambo ambayo yako kinyume na maadili, jambo ambalo ndilo linalomtenga mwanadamu na Mungu. Lakini wakati mwingi sisi huwa na sehemu fulani katika maisha yetu ambazo bado hatujaweza kukua. Basi kama haja ni kukua, hii ni kumaanisha kwamba huo ni upungufu.Upungufu huo hujidhihirisha kwa sisi kufanya makosa au kuwa na upungufu maishani mwetu, wa aina moja au nyingine.

Kwa mfano, Mkristo anaweza kukosa kuonekana kuwa mtu aliyejaa furaha na subira wakati anapopitia mambo magumu. Hili ni swala la kupungukiwa, au hata pengine la kufanya makosa. Lakini Mkristo wa kweli hatatoa visingizio kuhusu jambo hilo, badala yake yeye atamtafuta Bwana ili apate kukua katika sehemu hiyo ya maisha yake. Ndiposa mtoto wa Mungu hatambuliki kutokana na kupungukiwa kwake, bali yeye hujulikana kutokana na ushindi wake. Jambo kama hilo linaweza kugeuka na kuwa dhambi ikiwa mtu huyo ataamua kukubali kupungukiwa huko kuwe ni hali yake ya kudumu ya kiroho, na kukubali kuishi katika hali hiyo ya kupungukiwa na ukosefu huo wa neema maishani mwake.

2 Petro 3:18 inatufundisha “tukue katika neema”; nayo 2 Petro 1:5 inatuagiza kwamba, “katika imani yenu tieni na wema, na katika wema wenu maarifa.” Katika ujuzi wa maisha ya Mkristo, kuna hali ya mtu kuweza kukua, na kulingana na vile tunaendelea kumtumikia Bwana, ndivyo tunahitaji kuendelea kukua ili tuwe kama Kristo. Hata Huduma ya Kanisa ilijumuishwa katika mwili wa Kristo kwa “kusudi la kuwakamilisha watakatifu” (Waefeso 4:12). Hii ni kumaanisha kwamba Mkristo anazo sehemu fulani maishani mwake ambazo angali anahitaji kuendelea kukua ili apate kukamilika ndani yake Kristo.

Wana wa Israeli walikutana na vita nyingi wakati waliingia nchini Kanaani. Lakini ni kwa kulingana na vile walijitoa kwake Mungu, ndivyo walipata ushindi. Katika nchi hiyo kulikuwa kungali na majitu na miji iliyozingirwa na kuta kubwa, lakini wao walipata ushindi kwa nguvu zake Mungu kulingana na vile waliendelea kuwa watiifu kwa Mungu.

**JE, WAJUA?**

Huduma ya Uchunguzi (Probe Ministries) ilichapisha takwimu kutokana na ukaguzi ambao walifanya mwakani 2020, uliolenga Wamarekani 3,106 wenye umri wa kati ya miaka 18-55, ambao ulionyesha kwamba:

- Zaidi ya asilimia sitini (60%) ya vijana Wakristo (wa kati ya miaka 18-39) wanaamini kwamba Yesu, Budha, na nabii Mohamedi walikuwa wako sawa kama njia ya mtu kufuata ili apate wokovu.
- Asilimia thelathini (30%) ya Wanaprotestanti ambao wamezaliwa mara ya pili hawakuwa na uhakika kama Yesu alitenda dhambi alipokuwa duniani.
- Karibu asilimia themanini (80%) ya vijana wa dini ya Kikatoliki hawakuwa na uhakika ikiwa Yesu aliishi maisha yasiyokuwa na dhambi wakati alipokuwa duniani.

Neno Linalofaa kwa Msimu Huu

# WAKATI IMANI IMEINGIA SHAKA

*Mara Yesu akanyosha mkono wake, akamshika.* —Mathayo 14:31

Wakati chombo kilikuwa kikipigwa na mawimbi yaliyoandamana na upepo hapo katika masaa ya usiku wa manane, Yesu aliwajia huku akitembea juu ya maji. Wanafunzi wakaingiwa na hofu, wakidhani kwamba inawezekana ilikuwa ni pepo. Lakini Yesu akasema nao na kuwaambia, "Jipeni moyo ni mimi; msiogope" (Mathayo 14:27). Hii ilikuwa ni nafasi ya ajabu ya wao kusikia sauti ya Mwokozi, huku wakiwa wamo ndani ya mawimbi hatari ya maisha. Uwepo huo wa Bwana, na sauti hiyo yake, ni mambo ambayo yangali yanapenya hata kwenye mawimbi yetu ya maisha ya kisasa.



Lakini Petro alikuwa na shauku la kutembea majini kumwendea Kristo. Ndiposa Yesu akamwita aje kwake; basi hapo kwenye mawimbi Petro alichukua hatua na akatoka mtumbwini. Hili lilikuwa tendo kuu la imani na kumtumaini Yesu. Naye Petro akatembea majini huku akimwelekea Yesu. Hili likawa ni dhihirisho kuu la ushindi ambao unapatikana ndani yake Kristo. Mtume Petro akaweza kushinda nguvu za kawaida za maji kwa njia ya nguvu za Mungu. Basi hata wokovu uko hivyo, kwa sababu sisi tunawezeshwa kushinda nguvu za kawaida za dhambi katika maisha yetu, na kuweza kuishi maisha matakatifu kwa njia ya nguvu za Mungu.

Lakini wakati Petro alikuwa akitembea majini, alitazama huku na huko na kuona nguvu na ukali wa dhoroba iliyomzunguka. Na uhalisi wa hatari iliyokuwako ulifanya imani yake kuingia shaka, na papo hapo akaanza kuzama majini. Lakini kabla ya kushindwa kabisa yeye alimlilia Bwana. "Mara Yesu akanyosha mkono wake, akamshika" na Yesu naye akamkemea kwa ajili ya ukosefu wake wa imani. Na wakati waliingia chomboni, dhoruba hiyo ikakwisha mara moja.

Ushindi ni kitu cha ajabu! Mtu kupata ujuzi wa nguvu za kiungu za Mungu ambazo zinamwezesha kushinda dhambi na ulimwengu huwa ni baraka ya kimuujiza. Lakini kuna wakati ambapo dhoruba inaweza kuwa kali sana; na kama sisi hatutakuwa waangalifu, hata nasi imani yetu inaweza kuanza kuingia shaka. Lakini hakuna haja ya sisi kuzama, mradi tutadumisha macho yetu kwake Yesu. Na tunapojipata kwamba imani yetu imeanza kuingia shaka, wakati nguvu za ulimwengu na za mwili zinapoanza kutuvuta sana, tunaweza kumlilia Bwana, na Yeye atatuinua; kwa maana hiyo ndiyo hali halisi ya Mwokozi wetu.

Na ikiwa Bwana atanyoosha mkono wake kwetu, wakati huo ambapo imani yetu imeanza kuingia shaka, tutawezaje kukosa kufanya vivyo hivyo wakati ndugu na dada zetu (katika Bwana) wako katika hali kama hiyo? ■

Anwani

The Gospel Truth
P. O. Box 2042
Nixa, MO 65714
USA

Email:
editor@thegospeltruth.org

Utakatifu kwa Bwana